# STARLINK | MWONGOZO WA USANIDI WA PERFORMANCE



## Kilicho Ndani ya Kasha



Sahani ya Starlink Performance



Kigawi Mahiri cha Umeme



Kebo ya
Starlink Performance

Mita 25
(futi 82)



Kebo ya
Ethaneti ya Starlink

Mita 5
(futi 16.4)



Kebo ya
Umeme wa AC ya Starlink

Mita 1.5
(futi 4.9)



Kebo ya
Umeme wa DC ya Starlink

Mita 1.5
(futi 4.9)

## 1 | Pakua Programu ya Starlink

Pakua Programu ya Starlink na uchanganue msimbo wa QR ili upitie mchakato wa kufunga.




setup.starlink.com




## 2 | Chomeka Kebo na Uunganishe kwenye Umeme

Fungamanisha ncha ya Kiunganishi cha Performance ya kebo ya Starlink iliyoonyeshwa kwa alama nyekundu na uichomeke kwenye Starlink yako kwa kushikilia ncha ya plagi na kuingiza kabisa kwenye sahani.

Unganisha ncha ya pili ya kebo ya Starlink kwenye kigawi cha umeme. Funga ama Kebo ya Umeme wa AC (2A) au DC (2B) ndani ya kigawi cha umeme, kulingana na chanzo chako cha umeme, na uchomeke ndani ya soketi ya umeme. Hakikisha kebo zote zimechomekwa kikamilifu hadi uso wa plagi uwe sambamba na sehemu ya juu.

Ikiwa inahitajika, ili kuondoa kebo ya Starlink, zungusha kola kinyumenyume kisha uivute ili kuichomoa kutoka kwenye Starlink yako.






## 3 | **Tafuta Eneo la Kufunga na Ufungamanishe Starlink**

Starlink yako inahitaji mwonekano wazi wa anga ili iweze kuendelea kuunganishwa na setilaiti zinaposonga juu. Vitu vinavyozuia muunganisho kati ya Starlink yako na setilaiti, kama vile tawi la mti, mlingoti, au paa, vitasababisha ukatizaji wa huduma. Tumia zana ya kizuizi iliyo kwenye Programu ili kuhakikisha umechagua eneo linalofaa la kufunga.

Arifa kwenye Programu itaonyesha ikiwa unahitaji kuzungusha Starlink ili ifungamanishwe vizuri. Gusa arifa ili kutumia zana ya kufungamanisha. Hakikisha unaangalia vizuizi na Starlink yako imefungamanishwa vizuri kabla ya kufunga Starlink yako kabisa.



## 4 | **Unganisha Starlink**

Ikiwa unatumia Ruta ya Starlink, unganisha Ruta kwenye Kigawi Mahiri cha Umeme kwa kutumia kebo iliyotolewa kwenye seti ya ruta. Pitia mchakato wa kufunga Starlink kwenye Programu ya Starlink. Unaweza kutumia Programu ya Starlink ili kuona takwimu, kufikia mipangilio ya kifaa na kuwasiliana na kituo cha usaidizi.

Ikiwa unatumia ruta ya mhusika mwingine, tumia kebo ya ethaneti iliyotolewa katika Seti ya Performance. Baada ya kuweka ruta yako ya mhusika mwingine na kuunganisha kwenye Starlink kwa tundu la WAN, fungua programu ya Starlink. Programu ikisema "Starlink haifikiki", unda njia isiyobadilika katika mipangilio ya usanidi wa ruta yako.

Tafadhali rejelea hati za ruta yako ili upate maelekezo kuhusu kuweka njia isiyobadilika.
Kituo cha mtandao: 192.168.100.0
Kitambulishi cha Mtandao Mdogo: 255.255.255.0
Lango: 192.168.100.1
Kiolesura: WAN
Kumbuka: Machaguo haya yanaweza kutofautiana kulingana na zana na vifaa vyako mahususi na usanidi wa mtandao.



## KIGAWI MAHIRI CHA UMEME

### 1 | **Ondoa Kiunzi**

Ondoa kigawi cha umeme kutoka kwenye kiunzi kwa kuvuta na kupindisha pini za kutolewa haraka katika mwelekeo wowote. Pini zitafungwa mahali pake ili kuwezesha kuondolewa kwa urahisi kwa kigawi cha umeme.




### 2 | **Tia Alama kwenye Matundu ya Kuelekeza**

Chagua eneo la kufunga lisilozidi umbali wa mita 1.5 (futi 5) kutoka kwenye chanzo chako cha umeme.

Tia alama kwenye eneo la matundu manne kwenye kiunzi cha kigawi chako cha umeme ukitumia kalamu au penseli.



## 3 | **Toboa Matundu ya Kuelekeza**

Toboa matundu hayo kwa msumari wa keekee wa milimita 8 (inchi 5/16).




## 4 | **Funga Nanga na Kiunzi**

Sukuma nanga kwenda ndani ya matundu hadi zisawazishwe na ukuta. Weka kiunzi cha ukutani juu ya nanga kisha ufunge kiunzi hicho kwenye ukuta kwa kutumia skurubu hadi kishikilie vizuri.



## 5 | **Chomeka Kebo na Ufunge Kigawi cha Umeme**

Chomeka kebo za Starlink, ethaneti na za AC au DC ndani ya kigawi cha umeme kwa kuondoa plagi zisizopenya maji na uhakikishe kebo zimechomekwa kikamilifu. Sukuma kigawi cha umeme kiingie kwenye kiunzi, na uhakikishe pini zote za kufunga zimeingia mahali pake.

Kamilisha ufungaji kwa kuelekeza kebo ya Ethaneti hadi eneo ulikofunga ruta, unganisha kwenye ruta kisha uchomeke ruta na kigawi cha umeme kwenye chanzo chako cha umeme.

